

**SALAAM ZA KATIBU TAWALA - ARUSHA DKT. TOBA ALNASON  
NGUVILA, KWA KATIBU MKUU KIONGOZI MHE. BALOZI DKT. MOSES  
MPOGOLE KUSILUKA, WAKATI WA KUFUNGUA KIKAO KAZI CHA  
SITA (6) CHA SERIKALI MTANDAO FEBRUARI 17, 2026 KATIKA  
UKUMBI WA AICC ARUSHA.**

---

**Mhe. Balozi Dkt. Moses Kusiluka;** Katibu Mkuu Kiongozi

**Ndg. Mululi Mahendeka;** Katibu Mkuu Ikulu

**Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya**

*Dkt. Mussa Kisaka; Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

*Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.*

*Mhandisi. Benedict Ndomba; Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA),*

*Wakurugenzi wa Halmashauri, Mashirika na Taasisi Mbalimbali,*

*Wakuu wa Idara za TEHAMA na Watumishi kutoka Taasisi mbalimbali*

*Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Watumishi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao;*

**Viongozi wa Dini,**

**Waandishi wa Habari,**

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na baraka, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo katika Kikao Kazi hiki cha Sita (6) cha Serikali Mtandao.

**Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi,**

Ninafuraha kubwa kukukaribisha katika Mkoa wa Arusha, hususan katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa AICC, ambako kikao hiki kinafanyika kwa muda wa siku tatu kuanzia leo tarehe 17 hadi 19 Februari, 2026. Tunatambua majukumu yako mazito ya kitaifa, lakini uwepo wako hapa unaonesha dhamira yako ya dhati ya kuimarisha na kuijenga Serikali Mtandao nchini.

Napenda pia kuwashukuru viongozi wote wa Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma na Binafsi, Watumishi wa Serikali, Wadhamini, Viongozi wa Dini pamoja na Waandishi wa Habari kwa kushiriki nasi katika kikao hiki. Karibuni sana Arusha, jisikieni mpo nyumbani!

### **Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Napenda kuipongeza Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) kwa maandalizi mazuri ya Kikao Kazi hiki cha Sita na kwa kuendelea kuliadini Jiji la Arusha kuwa mwenyeji wa vikao hivi. Wakazi wa Mkoa wa Arusha tunajivunia heshima hii na tunawashukuru sana e-GA kwa kutupatia fursa hii muhimu.

Mkoa wa Arusha ni miongoni mwa wadau wakuu wa Serikali Mtandao, tumekuwa watumiaji wazuri wa mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi wa wa kila siku na utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kipekee, napenda kuipongeza e-GA kwa jitihada zake za kutoa huduma mbalimbali za serikali mtandao, ikiwemo kuunganisha mifumo ya TEHAMA Serikalini kupitia Mfumo wa Ubadilishanaji Taarifa Serikalini (GovESB), ambao umeongeza ufanisi wa utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi.

### **Mhe. Katibu Mkuu Kiongozi;**

Mkoa wa Arusha unaunga mkono kikamilifu jitihada za Serikali Mtandao kama sehemu ya utekelezaji wa dhamira ya **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan** ya kujenga Serikali ya Kidijitali.

Ni rai yangu kwa Taasisi zote za Umma zilizopo mkoani Arusha kuendelea kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao, ili Mkoa wetu uwe mfano bora na kinara wa matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kwa kumalizia, napenda kukushukuru tena Ndugu Mgeni rasmi. **Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi**, viongozi na wageni wote mliohudhuria kikao hiki. Kwa heshima hii

kubwa, tunakuahidi kuwa watendaji na washiriki wote waliopo hapa tutasimamia kwa vitendo maelekezo utakayotupatia.

Nawakaribisha kutembelea vivutio mbalimbali vya utalii vilivyopo ndani ya mkoa wetu. Karibuni sana Arusha!

Asanteni sana kwa kunisikiliza.

**Kwa pamoja, tuijenge Serikali Mtandao kwa vitendo.**

**Kazi na Utu.....**